

HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI



TAARIFA KWA UMMA.

Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni leo Jumatano, Mei 22, 2019 katika Mkutano wake wa Kawaida wa Baraza la Madiwani. Robo ya tatu, uliofanyika Katika Ukumbi wa Manispaa, Pamoja na Mambo mengine limethibitisha matumizi ya jumla ya **Tshs.28,210,534,383.00** sawa na asilimia **81.45** ya lengo ambapo **Tshs.8,512,983,875.00** zimetumika katika maeneo yasiyo ya Ruzuku na **Tshs.19,697,550,508.00** zimetumika katika maeneo ya Ruzuku ikihusisha **Tshs.11,511,620,774.09** za mishahara, **Tshs.480,095,362.12** za matumizi mengineyo na **Tshs.7,705,834,421.79** zilizotumika kutekeleza Miradi ya maendeleo kwa kipindi cha Januari hadi machi, 2019.

Katika Mkutano huo wa kawaida wa Baraza la Madiwani Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni pia imetekeleza agizo la Serikali kuu la Kushughulikia masuala ya Watumishi ambapo watumishi **56** wamethibitishwa kazini, watumishi **410** wamepandishwa vyeo na Watumishi **17** wamerekebishiwa miundo ya utumishi wao kwa kuzingatia Sheria zinazohusu Utumishi wa Umma.

Aidha Baraza la Madiwani limethibitisha taarifa za utekelezaji wa kazi za Kamati za Kudumu za Halmashauri yaani Kamati ya Huduma za uchumi Afya na Elimu, Kamati ya Mipangomiji na Mazingira, Kamati ya Maadili, Kamati ya Kudhibiti Ukimwi na Kamati ya Fedha na Uongozi zilizofanyika katika robo ya tatu kuanzia mwezi Januari hadi Machi 2019.

Imetolewa na:-

Sebastian Modestus Mhowera

**AFISA UHUSIANO WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI.**